# OPENER STD 8 TERM 2 2020
# KISWAHILI

NAME......................................................................................

Learner's Number ☐☐☐

Gender Boy ☐ Girl ☐

County name ............................................ County code ☐☐☐

Sub county name ............................................ Sub county code ☐☐☐

School name ............................................School code ☐☐☐

The grid below is to be filled by the teacher after marking the learner's work

| | Level 1 | Level 2 | Level 3 | Level 4 |
|---|---|---|---|---|
| Numbers 1-15 | | | | |
| Measurement 16-23 | | | | |
| Geometry 24-25 | | | | |

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.***

Sekta ya elimu imepokea mabadiliko _______**1**_______ sana tangu _____**2**_____ kwa mfumo wa 8-4-4. ______**3**_______ mabadiliko haya yanamwathiri mlengwa _____**4**_____ ambaye ni mwanafunzi huku mengine yakiwaathiri _____**5**____ wengineo kama vile walimu, wazazi na jamii. Tangu mtaala wa umilisi _____**6**______, baadhi ya walimu wamekumbwa na changamoto ______**7**______. _______**8**_______, mafunzo yanazidi kutolewa kupitia makongamano mbali mbali nchini _____**9**______.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. nyingi | B. chache | C. makubwa | D. kutwa |
| **2.** | A. kutupiliwa | B. kutupwa mbali | C. kutupwa | D. kutupiliwa mbali |
| **3.** | A. Badala ya | B. Baadhi ya | C. Pamoja na | D. Kulingana na |
| **4.** | A. hasa | B. sana | C. haswa | D. sanaa |
| **5.** | A. mshikadau | B. wakufunzi | C. wadau | D. wataalamu |
| **6.** | A. ilipoanzishwa | B. ulipobunishwa | C. ulipobuniwa | D. ilipotambulishwa |
| **7.** | A. haba | B. si haba | C. mingi | D. wengi |
| **8.** | A. Hata hivyo | B. Kwa hivyo | C. Hivyo basi | D. Hivyo |
| **9.** | A. yote | B. mote | C. pote | D. kote |

Kurwa na Doto walikuwa ndugu wa toka nitoke. Walifanana kama _____**10**_____. Ilikuwa vigumu kwa _____**11**_____ kuwatofautisha. Hata hivyo, walikuwa maskini sana. Asubuhi wangerauka shambani bila kufungua ______**12**______. Kama si bidii yao, _____**13**_______ kujikimu maishani. Hata hivyo, siku moja _______**14**_______ iliwashukia. Walipata utajri wasioulalia wala ______**15**_______.

**10.** A. sahani na kawa B. shilingi kwa ya pili
C. pua na mdomo D. kinu na mchi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. yeyote | B. yoyote | C. wowote | D. chochote |
| **12.** | A. kikombe | B. sahani | C. kinywa | D. kiamshakinywa |
| **13.** | A. hawangeweza | B. hawangeliweza | C. wasingeweza | D. wasingaliweza |

**14.** A. giza totoro B. joka la mdimu
C. dhoruba kali D. nyota ya jaha

**15.** A. kuutandikia B.kuutafuta D. kuuchokea D. kuuamkia

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.***

**16.** Kanusha sentensi kwa ustadi
Mwana anayelelewa vizuri hufaulu maishani.
A. Mwana asiyelelewa vizuri hafaulu maishani.
B. Mwana anayelewa vizuri hafaulu maishani.
C. Mwana asipolelewa vizuri hafaulu maishani.
D. Mwana asiyelelewa vizuri hufaulu maishani.

**17.** Andika usemi wa taarifa wa:
"Safari yetu itaanza kesho," baba akasema.
A. Baba alisema kuwa safari yetu ni ya siku ifuatayo.
B. Baba alisema kuwa safari yao ingeanza siku iliyofuata.
C. Baba alisema kuwa safari yetu ingeanza keshoye.
D. Baba alisema kuwa safari yao itaanza siku iliyofuata.

**18.** Chagua jibu lenye nomino iliyo katika ngeli ya **LI-YA**
A. Mshauri B. Mswaki
C. Maneno D. Nywele

**19.** Chagua methali ambayo inaafikiana na maelezo haya.
Tunapaswa kujisaidia kwa vile vitu tulivyo navyo wala hatupaswi kutamani vingi tusivyo navyo.
A. Ukiona vyaelea jua vimeundwa.
B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
C. Mtu hujikuna ajipatapo.
D. Mui huwa mwema.

**20.** Panga maneno yafuatayo vizuri kulingana na kamusi.
***(i) Mwandishi*** ***(ii) Muktubi***
***(iii) Mwashi*** ***(iv) Msamaria***
A. iv, ii, i, iii B. ii, iv, i, iii
C, ii, iv, iii, i D. ii, i, iii, iv

**21.** Chagua sentensi yenye **kwa** ya sababu.
A. Wakubwa kwa wadogo.
B. Waliadhibiwa kwa kutohudhuria darasa.
C. Mtoto alinyolewa kwa wembe mkali.
D. Nyumbani kwao kuna ngombe wengi.

**22.** Wingi wa sentensi :Mtumbwi huyu mpya ni wa mvuvi yule.
A. Mtumbwi huu mpya ni wa wavuvi wale.
B. Mitumbwi hii mipya ni ya wavuvi wale.
C. Mitumbwi hii mipya ni ya mvuvi yule.
D. Mitumbwi hizi mpya ni za wavuvi wale.

**23.** **Kipeto** ni kwa barua ilhali **shehena** ni kwa
A. nyuki B. maua
B. nywele D. mizigo

**24.** Ni ipi si aina ya shairi?
A. Ngonjera B. Kibwagizo
C. Tarbia D. Tathlitha

**25.** Maana ya **"ungalifika ungalinisaidia"** ni
A. ulifika lakini hukunisaidia
B. ulifika na ukanisaidia
C. hukufika wala hukunisaidia
D. hukufika ila ulinisaidia

**26.** Kitenzi **soma** katika kauli ya kutendea ni
A. somesha B. somea
C. someka D. somasoma

**27.** Kamilisha methali;
Siri ya mtungi
A. aijuaye chungu B. aijuaye debe
C. aijuaye kata D. aijuaye kopo

**28.** Chagua sentensi iliyotumia kiashiria kisisitizi.
A. Mambo hayo hayo hayafai kuambiwa watoto.
B. Jarida lili hili la leo ndilo linalovutia.
C. Shule hiyo hiyo unayozungumzia si ya bweni.
D. Mbuzi wa borana Ali ndiye yule.

**29.** Ndugu wa kike wa baba ni
A. shangazi B. mwamu
C. halati D. wifi

**30.** Anayewatunza wanyama wanaopandwa ndiye
A. sarahangi B. hamali
C. saisi D. kuli

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***

Binadamu amekuwa na tabia za kustaajabisha sana. Utu wa mja umeadimika na kuwa adimu kama kaburi la baniani. Hivyo ni kusema kuwa, vitendo vyake vimekuwa vya kushangaza na kuacha wengi midomo wazi kama mapango ya visiki.

Hivi majuzi kuliripotiwa mwanamume mmoja kwa jina Bwaka aliyembaka bintiye wa miaka tisa aliyekuwa mwanafunzi wa darasa la nne. Ilisemekana kuwa janadume hilo lilifanya kitendo hicho cha kusikitisha saa tatu usiku ambapo mke wake alikuwa amechelewa kurudi toka sokoni. Katika kukurukakara za kumnasua msichana huyo mdogo mikononi mwa mzee huyo, polisi waliwasili ghafla bin vuu. Polisi waling'amua kuwa, bwana huyo alikuwa amepiga mtindi kupindukia.

Majirani waliokuwa na ghadhabu mithili ya mkizi walimpa **shaibu** huyo mkongojo wa mbwa kuingia msikitini. Jamaa huyo alitiririkwa na machozi lakini hiyo ilikuwa bure bilashi mbele ya umati uliojaa hasira. Waliosema kuwa hasira ni hasara hawakukosea kwani baada ya muda kiasi katika ile vuta nikuvute ya waja na walinda usalama, mzee huyo alifungua pijo nambari miguu niponye kuokoa maisha, huku jirani mmoja akiwa amejeruhiwa vimbaya

Askari walilipua gesi za kutoa machozi ili watu wafumukane lakini juhudi zao **ziliambulia kidole gutu**. Haikuweza kubainika vizuri alikojificha lakini msako uliendelea katika majengo yaliyokuwa karibu. Waliokuwa wamelala waligutushwa na fujo hizo pamoja na milio ya bunduki kila mahali.

Baada ya muda wa koo kumeza punje, jamaa huyo alitiwa mbaroni na moja kwa moja akapelekwa katika kituo cha polisi kujibu mashtaka. Ilifahamika kuwa mzee huyo wa umri wa makamo alikuwa amekosana na mkewe siku mbili zilizopita na hakuwa na budi kufanya jambo hili kujiridhisha na kujifurahisha nafsi yake.

Jamani ! Mtoto uliyemzaa mwenyewe unawezaje kumfanyia kitendo kama hiki bila huruma? Dunia inaelekea wapi? Sielewi kama mambo haya yatafika mwisho. Naomba serikali ikabiliane na majanga kama haya kwa kutoa adhabu itakayowafanya wasiweze kufikiria vitendo kama hivi abadan katan. Iwapo binadamu atakuwa msalihina, mambo kama haya yatakoma kabisa.

31. Kulingana na habari, tabia za kustaajabisha zinatokana na
   A. utu ulioadimika kama kaburi la baniani
   B. vitendo visivyo vya kawaida vya kinyama
   C. kufanya mambo shelabela kwa binadamu
   D. mazingira mabaya

32. Mwanamume aliyedaiwa kumbaka bintiye yake alifanya hivyo kwa kuwa
   A. mkewe alichelewa kutoka sokoni
   B. alitaka kuifurahisha nafsi yake
   C. alikuwa amelewa chakari
   D. alikuwa na hasira kwa kukosana na mkewe

33. Katika purukushani za kumwadhibu mhalifu, hasara ilitokea kwa nani?
   A. Jirani mmoja ambaye jina lake halijatajwa.
   B. Askari aliyekuwa na hasira ya mkizi.
   C. Mhalifu aliyekimbizwa na askari.
   D. Mama wa mhasiriwa.

34. Badala ya kusema juhudi zao **<u>ziliambulia kidole gutu</u>**, mwandishi angesema
   A. bidii zao zilikuwa chache.
   B. juhudi zao zilienda mrama.
   C. juhudi zao zilikuwa ovyo.
   D. juhudi zao hazikufua dafu.

35. Ni nini maana ya moja kwa moja kama ilivyotumika katika habari?
   A. Kwenda kwa mwendo wa kasi.
   B. Mwendo wa bega kwa bega.
   C. Kwenda haraka bila kupitia mahali pengine.
   D. kuchanganya miguu.

36. Chagua kauli isiyo sahihi kulingana na ufahamu.
   A. Binti aliyebakiwa alikuwa na miaka minane.
   B. Mwandishi anaomba wito wa serikali kukabiliana na majanga ya aina hii.
   C. Mbakaji aliitwa Bwaka.
   D. Idadi ya polisi waliomshika mbakaji haijulikani.

37. Ni kipi kisawe cha **shaibu**?
   A. Buda
   B. Ajuza
   C. Shahibu
   D. Matatizo

38. Kwa kuwa hasira ni hasara, hasara katika aya ya tatu ilimpata nani?
   A. Msichana aliyebakwa
   B. Mbakaji aliyetajwa
   C. Jirani mmoja ambaye hakutajwa
   D. Afisa wa polisi

39. Ni kwa nini maafisa wa polisi walilipua vitoza machozi?
   A. Ili watu wasambaratike.
   B. Ili watu wajumuike.
   C. Ili kuwatoa machozi waliokuwapo
   D. Ili kumwadhibu mhalifu.

40. Ni gani si sahihi kulingana na aya ya mwisho?
   A. mwandishi ana uhakika wa mwisho wa majanga.
   B. Huenda sala ikakomesha unyama.
   C. Mwandishi ana imani na serikali.
   D. Mwandishi anaonyesha hali ya kuchanganyikiwa.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.***

Tangu jadi, usawa wa jinsia umekuwa suala muhimu katika jamii nyingi. Kubaguana kwa misingi ya kijinsia kumekita katika jamii nyingi. Ubaguzi huu umejadiliwa katika **ngazi** nyingi. Jambo linalojitokeza katika mjadala huu ni kuwa ubaguzi huu haufai.

Tamaduni nyingi nchini Kenya zinawadunisha wanawake kwa kuendelea kushikilia kukeketwa kwa watoto wa kike pindi tu **wanapovunja ungo**. Madhara ya utamaduni huu ni mengi. Kwanza imethibitishwa kuwa wanaokeketwa hudhurika kiafya. Wengi hupata matatizo baadaye wanapojifungua. Mara nyingi vifaa visivyofaa kutumika. Uwezekano mkubwa wa kuambukizana magonjwa miongoni mwa wanaokeketwa upo. Aidha wengi huvunja damu sana.

Ubaguzi wa kijinsia hujitokeza masomoni. Imethibitishwa kwamba katika elimu idadi kubwa ya wanafunzi huwa wa kiume. Je, wanafunzi wa kike huwa wapi? Wengi huozwa mapema na wengine huwa walezi wa wanuna wao, kwa hivyo hubaki nyumbani.

Isitoshe, wanawake mara nyingi hubaguliwa kikazi. Kwa mfano, ni nadra sana kumwona mwanamke akiendesha matwana. Hata katika idara kuu za serikali, wakurugenzi wengi ni wanaume. Usawa ni jambo muhimu. Nchi zilizoendelea hupiga vita ubaguzi wa kijinsia. Katika nchi hizo, nafasi hutolewa katika hali ya usawa.

Mtoto wa kike pia hukabiliwa na dhuluma ya kunajisiwa. Unyama huu huu huwaacha ho . **Mara nyingi wanaotekeleza unyama huu huwa jamaa zao**. Wengi hawafikishwi mahakamani kwa kisingizio kuwa kosa lililofanywa ni la kifamilia na litatatuliwa kifamilia. Hata wanaofikishwa mahakamani huishia kuachiliwa huru kutokana na ukosefu wa ushahidi.

Nafasi ya mwanamke nchini imejitoa kimasomaso hivi kwamba ni rahisi mno kuitathmini. Idadi kubwa ya wanawake imejisalimisha kwa woga. Kundi hili hushikilia dhana potovu kuwa hali yao iliamuliwa na maumbile. Nafasi zao ni za nyumbani hasa jikoni. Si kawaida kuwaona katika kumbi za tafrija. Wao hubaki nyumbani wakiwatunza watoto.

Aidha mwanamke ndiye mpishi nyumbani. Jamii nyingi huichukulia kuwa upishi unafaa kufanywa na wanawake. Hata wana wa kiume hukataa katakata kuwasaidia dada zao katika shughuli za mekoni. Hapa ndipo mbegu za taasubi hupandwa na kupaliliwa.

Wakati umefika wa mwanamke kujinasua kutokana na tamaduni zilizopitwa na wakati. Siku hizi wanawake wana vielelezo bora maishani.

41. Tangu jadi
A. usawa wa jinsia umepingwa katika jamii.
B. watu wamebaguliwa kwa misingi ya jinsia.
C. suala la jinsia lilijadiliwa na kupata suluhu.
D. watu walihimizwa wabaguane kijinsia.

42. Neno **ngazi** kulingana na ufahamu lina maana ya
A. daraja la kupandia.
B. kitu cha kuvukia.
C. vikao vya kimataifa.
D. viwango mbalimbali.

43. Mijadala mingi inayoandaliwa
A. hupinga sana usawa wa jinsia.
B. hutetea ubaguzi wa jinsia.
C. huisha bila mapendekezo kutolewa.
D. hutetea sana usawa wa jinsia.

44. Maana ya **wanapovunja ungo** ni
A. wanapokeketwa.
B. wanapovunja uteo.
C. wanapokomaa.
D. wanapomaliza masomo.

45. Madhara yapi hayawezi kusababishwa na ukeketaji?
A. Kupata shida wakati wa kujifungua.
B. Maradhi ya zinaa.
C. Kuvunja damu nyingi.
D. Kuozwa kabla ya wakati.

46. Wanawake kuwa wachache katika nyadhifa mbalimbali ni ishara kuwa
A. hawayawezi majukumu mazito.
B. uwezo wao unatiliwa shaka.
C. wanaume ndio wengi nchini.
D. wanaume wengi wamesoma sana

47. **Mara nyingi wanaotekeleza unyama huu huwa jamaa zao**. Chagua methali inayolingana na maelezo haya?.
A. Kikulacho ki nguoni mwako.
B. Zimwi likujualo halikuli likakumaliza.
C. Damu ni nzito kuliko maji.
D. Akikalia kigoda mtii.

48. Kesi nyingi za ubakaji hutupiliwa mbali kwani
A. jamii hutaka zisuluhishwe kwa maelewano.
B. mahakama hukataa kuzishughulikia.
C. aghalabu washukiwa hutoa hongo.
D. kesi zenyewe hukosa ushahidi wa kutosha.

49. Ubaguzi hujitokeza katika haya yote ila
A. ugavi wa majukumu.
B utoaji wa ajira.
C. machweo ya burudani.
D. wakati wa maakuli.

50. Kichwa kifaacho makala haya ni
A. Ajira za watoto.
B. Madhara ya ukeketaji.
C. Usawa wa jinsia.
D. Elimu ya wasichana.